**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA.**
**FOMU YA MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA ,2021.**

SHULE YA SEKONDARI MCHUCHUMA
S.L.P 43,
**LUDEWA.**

TAREHE______________

Kumb na. MCHSS/LDC/JOIN____________

MZAZI/MLEZI WA ________________________
S.L.P________

Ndugu,

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2021**

## 1.0. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kwa masomo ya sekondari kidato cha kwanza kwa mwaka 2021 nakupongeza kupata fursa hii adhimu.

### 1.1. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Mchuchuma ipo umbali wa KM 44 kusini mashariki mwa Mji Ludewa. Ipo katika kata ya Luilo, wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe. Ni shule ya kutwa na ni shule ya mchanganyiko yaani wavulana na wasichana.

### 1.2. TAREHE YA KURIPOTI SHULENI.

Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza wa masomo tarehe ______________, unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo bila kukosa.

### 1.3. HUDUMA ZA ZILIZOPO SHULENI

a. Maji ya bomba
b. Umeme (TANESCO)
c. Hosteli kwa wasichana (wavulana wana utaratibu maalumu)
d. Chakula milo yote mitatu (uji, ugali, wali kwa maharage)

## 2.0. MAMBO YA KUZINGATIA

### 2.1. SARE ZA SHULE

Shule ina sare za aina mbili nazo ni:

i. Sare wakati wa masomo darasani.
ii. Sare baada ya masomo darasani.

Scanned with CamScanner

I. **SARE WAKATI WA MASOMO DARASANI**

- **WAVULANA**
  - Suruali nyekundu (damu ya mzee) yenye rinda mbili (selebration) iliyopinuwa chini (16 size). Itavaliwa kuanzia jumatatu hadi jumatano.
  - Suruali ya kijivu. Itavaliwa kuanzia alhamisi hadi ijumaa.
  - Shati jeupe mikono mirefu (mawili).
  - Kiatu cheusi cha kamba na kisigino kifupi.
  - Soksi nyeusi.

- **WASICHANA**
  - Suruali nyekundu (damu ya mzee) yenye rinda mbili (selebration) iliyopindwa chini (16 size). Itavaliwa kuanzia jumatatu hadi jumatano.
  - Suruali ya kijivu. Itavaliwa kuanzia alhamisi hadi ijumaa.
  - Kigauni cheupe chenye marinda na mikono mirefu (kisolo) au (koshibo) urefu kufikia magoti.
  - Kiatu cheusi cha kamba na kisigino kifupi.
  - Soksi nyeupe.

**NB**: Andaa fedha, mafundi watapatikana shuleni watakaopewa vipimo vinavyohitajika.

II. **SARE BAADA YA MASOMO DARASANI**

**WOTE**

- Track suit za rangi ya light blue ndiyo itakayotumika darasani kabla hujapata sare ya darasani (isibane mwili).
- Gauni ya rangi ya dark blue kwa wasichana.

**2.2. NGUO ZA MICHEZO**

- Aje na T-shirt ya rangi ya njano na kaptura rangi ya blue.
- Kiatu cha michezo na soksi ndefu rangi ya blue au kijani.

**NB: HAIRUHUSIWI KWA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI MICHEZO, LABDA AWE NA KIBALI KUTOKA KWA DAKTARI.**

**2.3. VIFAA VYA DARASANI**

a) Uje na madaftari makubwa (Counter books) tisa (9).
b) Madaftari ya mazoezi 9, kwa ajili ya masomo 9.
(English, Kiswahili, History, Basic Mathematics, Geography, Civics, Biology, Chemistry na Physics).
c) Uje na kalamu za wino (nyeusi na bluu) za kutosha na kalamu za risasi na rula.
d) Uje na mkebe.
e) Uje na kiti (makubaliano kikao cha wazazi).

Scanned with CamScanner

## 2.4. VIFAA VYA USAFI

- Uje na ndoo ya plastiki pamoja na sabuni za kutosha kwa ajili ya usafi wako binafsi.
- Uje na ufagio wa chelewa na na jembe au fyekeo kwa ajili ya kulimia bustani ya mboga na kwaajili ya kufanyia usafi. Jembe hilo ni mali yako haitakuwa mali ya shule.

## 2.5. HUDUMA YA HOSTELI

### 2.5.1 CHAKULA

Wanafunzi wanakula milo yote mitatu (3) shuleni. Hivyo unatakiwa kuja na michango kwa ajili ya chakula kama ifuatavyo:

i. Mahindi madebe 8 kwa mwaka.
ii. Maharage madebe 2 (Kg 40) kwa mwaka.
iii. Mchele sado 1 kwa mwaka.
iv. Fedha Tshs 40,000/= kwa ajili ya mpishi, kusaga,sukari, chumvi, mafuta ya kupikia, vitunguu n.k

### 2.5.2 MALAZI

- Uje na godoro la futi $2^1/_2$ kwa ajili ya kulalia.
- Uje na chandarua.
- Uje na sahani na kikombe kwa ajili ya chakula.

### 2.5.3 USALAMA WA VIFAA

- Unashauriwa kununua sanduku la bati (Trunker) pamoja na kufuri kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako vyote.

# 3.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE ZA SEKONDARI

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini pamoja na maelekezo kutoka Wizara ya Ofisi ya Rais – Tamisemi inayosimamia uendeshaji wa Elimu nchini. Utekelezaji wa sheria, miongozo, kanuni na maelekezo kutoka ngazi hizo unasimamiwa kwa pamoja shuleni na ofisi ya Mkuu wa shule, Baraza la walimu na Bodi ya shule.

**Unatakiwa kuzingatia kwa makini mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa kina mara ufikapo shuleni.**

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

Scanned with CamScanner

c. Kushiriki kikamilifu kufanya maandalio ya jioni ya masomo (preparation) na vipindi vya dini.
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazo pewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Kutunza mali za Umma.

## 3.1. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI.

i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
iii. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya
iv. Uvutaji bangi
v. Makosa ya jinai
vi. Kupiga au kupigana
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
viii. Kudharau bendera ya Taifa
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
xi. Kutoa mimba
xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
xiii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiv. Kuwa na simu ya mkononi

## 3.2. FOMU ZINGINE MUHIMU

Naambatanisha na fomu zifuatazo ambazo zitawasilishwa shuleni wakati wa kuripoti zikiwa zimejaza kikamilifu.

(i) Fomu ya maelekezo yako binafsi
(ii) Fomu ya vipimo kuhusu afya yako

Karibu sana katika shule hii.

Wako katika Ujenzi wa Taifa.

..............................

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
MCHUCHUMA SECONDARY SCHOOL
BOX 43 - LUDEWA

Scanned with CamScanner

# MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……………………………………………………………………
2. Mahali alipozaliwa ……………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………
4. Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………………………
5. Uhusiano wa mlezi ……………………………………………………………
6. Anuani ya mzazi/mlezi …………………………………………………………
7. Shule ya msingi ulikotokea ……………………………………………………
8. Dini ……………………………………dhehebu ……………………………
9. Mimi ……………………………………msichana/mvulana nimekubali kuingia kidato cha cha kwanza mwaka 2021 katika Shule ya Sekondari Mchuchuma na kwamba nitatumia fursa hii adhimu kwa juhudi na maarifa na nitakuwa mwaminifu kwa jamii na Taifa liloniwezesha kupata nafasi hii.
10. Nitatii sharia za shule na kanuni zote na nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi …………………………………… Tarehe ……………………

## 11. MAONI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MTOTO

Tafadhali eleza endapo kama kuna tatizo, jambo au tabia yoyote kuhusu mtoto ambayo Mkuu wa Shule anapaswa kufahamu

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

## 12. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Nimesoma maelezo yote na kuyaelewa vema . Hivyo nakubali kutekeleza maagizo yote kikamilifu. Pia nitazingatia Mwanangu kufuata taratibu zote za shule.

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………sahihi ……………………

Tarehe ……………………………………

Scanned with CamScanner

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

LUDEWA DISTRICT CUONCIL

MCHUCHUMA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 43,

LUDEWA.

To the Medical Officer,

..................................................

**PART A**

Mr/ miss ............................................................ (Name in full)

Please examine the above named pupil as to her/his physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should have to include the following categories:

1. Vision with/ without glasses right ........................................ left ....................................
2. Blood pressure ............................ Hemoglobin ..................................................................
3. P. V bleeding ........................................................................................................................
4. Urine for sugar, album and pregnancy .................................................................................
5. Stool for routine Examination ...............................................................................................
6. Venereal diseases ...................................................................................................................
7. Neurosis ..................................................................................................................................
8. Any abnormality of the:
   (a) Heart ........................................ (b) Lung ...........................................................
   (C)Speech .....................................................
9. Are there serious e.g. leprosy, epilepsy, asthma diabetes e.t .c ........................

Thank you

..............................................................................

**THE HEAD MASTER**

**PART B MEDICAL CERTIFICATE:**

(To be completed by an authorized Medical Officer)

(1) I have examined the named pupil and consider that he/she is fit physically and mentally for a full time schooling

(2) The comments

..........................................................................................................................................

Signature ................................................ Stamp ....................................

Scanned with CamScanner